

# Mng'ao Angavu huko Jamhuri ya Czech

*Imeandalawa na Sharon Goodrich, Majarida ya Kanisa*

Wakati mmoja nilipoteza glavu yangu ninayoipenda sana. Nilikuwa na huzuni sana. Mimi pamoja na mama yangu tulisali, lakini hatukupata. Nilijaribu kuwa na imani. Wiki moja baadae, kaka yangu mdogo aliipata glavu yangu mtaani! Mungu alijibu sala zetu. Ninampenda Yeye na ninajua anaishi.

Andre W., miaka 9



Sisi ni watoto wa Msingi katika Jamhuri ya Czech. Hivi ndivyo tung'aavyo kwa uangavu katika nchi yetu.

Ufukweni, wingu lilianza kuwa jeusi. Upopo ulivuma na kutengeneza mawimbi makubwa! Kulikuwa na ngurumo, radi na mvua ya mawe. Kila mtu alikimbia kujikinga. Hatukudhurika na dhoruba. Njiani kurudi nyumbani, tuliona pinde tatu za mvua. Tunajua kwamba Mungu alitusaidia na kutulinda.

Jakub B., miaka 10



Shuleni nina rafiki ambaye hakuna mtu mwagine anataka kuwa rafiki yake. Watoto wengine walianza kusema vitu vyta kejeli kwake ambavyo vilimfanya ajihisi mbaya. Nilimwambia mwalimu na nilimwalika rafiki yangu kucheza nami. Ilimfanya rafiki yangu kuwa na furaha!

Ludmila V., miaka 8



Nilimkasirikia mama yangu kwa sababu sikutaka kuoga na kwenda kulala. Siku iliyofuata nilijisikia vibaya kutokana na uchaguzi wangu mbaya. Mama alisema tunaweza kusali na kumwomba Baba wa Mbinguni atusamehe. Tulipiga magoti na kusali. Nilijihisi vyema. Nilijifunza kwamba tunaweza kutubu, na kwa sababu ya Yesu Kristo, tukasamehewa.

Samuel H., miaka 5



Nina marafiki shuleni amba si waumini wa Kanisa lakini amba bado wanaheshimu viwango vyangu. Kuna wakati nilisema lazima tusali, na walikubali! Nilikuwa mwenye furaha sana.

Ivana A., miaka 11




Mimi pamoja na rafiki zangu tulikuwa tukishuka ngazi. Wakati tulipofika kwenye lifti, nilipata hisia ambazo si za utulivu na nikawaomba rafiki zangu tusiitumie. Lakini waliamua kuitumia hivyo hivyo. Mimi nilitumia ngazi. Nilipofika



chini, rafiki zangu hawakuwepo pale. Lifti ilikuwa imekwama! Iliwachukua muda kabla hawajatoka nje. Nilikuwa na furaha kwamba hakuna madhara yoyote makubwa yalitokea. Pia nilihisi furaha kwamba nilimfuata Roho Mtakatifu.

Amalie N., miaka 10



Nilitoa ushuhuda wangu kanisani. Nilijipa ujasiri! Tangu wakati huo, nimemhisi Roho.

Eliska K., miaka 11



Wakati nguruwe wangu wa guinea alipoumwa, nilisali kwa ajili yake. Nina shukrani kwa Baba wa Mbinguni kwa sababu alitusaidia.

Aneta P., miaka 10



**TUTUMIE  
NYOTA!**

Tunakaribia kumaliza kukusanya nyota!  
Kama bado hujatuma nyota yoyote, harakisha na tutumie barua pepe ya picha ya nyota yako pamoja na hadithi yako, picha, na idhini ya mzazi katika liahona@ldschurch.org